# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 MjiniMagharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nitumie fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika chombo hiki tukufu cha kutunga sheria tukiwa wazima wa afya ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zao, hekima na busara katika kuiongoza Tanzania. Hakika utumishi wao umetukuka.

**Mheshimiwa Spika,**

Wazanzibari tunatembea kifua mbele na kujivunia kwa kasi kubwa ya maendeleo inayofanywa na Raisi wetu kipenzi, hii inadhihirisha kua tumemchagua mtu sahihi katika kulipaisha Taifa letu. Ibakie kutamka kua Mheshimiwa Raisi Hongera na tunakuhakikishia tutaendelea kukuunga mkono katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu. In Sha Allah.

**Mheshimiwa spika,**

Aidha, tunatoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Makamo wa kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa kushauriana vyema na Mheshimiwa Rais kwenye masuala mbali mbali ya uendeshaji wa nchi yetu.

**Mheshimiwa spika,**

Napenda kukushukuru na kukupongeza wewe na wasaidizi wako, mheshimiwa naibu spika na wenyeviti wa baraza kwa uongozi wenu mahiri katika kuliendesha baraza hili ambalo ni muhimili kati ya mihimili ya nchi . Mwenyezi mungu awazidishie hekima na busara na uwadilifu ili muweze kutekeleza vyema wajibu wenu.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazozichukuwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo na mabadiliko chanya katika sekta ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba pia kutumia nafasi hii kuwashukuru wakulima wetu kutoka sekta binafsi ya kilimo, kwa mchango wao mkubwa katika kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula na kuongeza uzalishaj wa mazao na mifugo kwa lengo la kumpatia chakula cha uhakika mwananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nitumie nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa kutekeleza majukumu yao vyema na naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo.

| | |
|---|---|
| Mhe. Mtumwa Pea Yussuf | Mwenyekiti |
| Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Makamo Mwenyekiti |
| Mhe.Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| Mh Mwantatu Mbarak Khamis | Mjumbe |
| Mhe Mihayo Juma Suleiman | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| Mhe Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| Mhe. Dk Mohammed Ali Suleiman | Mjumbe |
| Mhe Said Saleh Salim | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika,

Kamati hii inafanya kazi zake kwa karibu sana na makatibu watatu na msaidizi mmoja ambao ni:

| | |
|---|---|
| Ndg Asma Ali Kassim | Katibu |
| Ngd Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| Ndg Abubakar Mahmoud Iddi | Katibu |
| Ndg Azmina Khamis Hamad | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kuipitia bajeti hii, Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo na kushuhudia changamoto zinazoikabili miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia imepata fursa ya kutembelea maeneo ya wakulima ili kuona mafanikio na juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kuwasaidia wakulima na wananchi kwa ujumla. Kupitia ziara mbali mbali za kamati wajumbe tumeridhika na bajet ambayo imewasilishwa na tumetoa Baraka zote ili Waziri na wasaidizi wake warudi kwa wananchi ili kuwasaidia wakulima na wafugaji wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu ilianza kupitia bajeti ya Wizara hii kwa kuangalia mapato ya Wizara na taasisi zake mbali mbali ambazo zinakusanya mapato. Kwa kiasi kikubwa Kamati imeridhika na makadirio yaliotolewa kwa ukusanyaji wa mapato wa baadhi ya taasisi kama vile Idara ya misitu kwa kuanzisha vivutio vya utalii ambavyo vinasaidia ongezeko la pato la Taasisi na Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**

Kamati inaunga mkono juhudi na mikakati iliyowekwa na Wizara ya Kilimo yenye lengo la kuendeleza kilimo biashara ili kuzidisha uzalishaji wa mazao ya chakula. Mafanikio ya mikakati hii itakua ndio chachu ya kuongeza uzalishaji na hatimae itapunguza utegemezi wa chakula kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Wizara hii ya Kilimo katika usimamizi wa rasilimali za misitu ya hifadhi na ile misitu ya jamii. Kwani tumeshuhudia kupungua kwa uhalifu katika maeneo yetu ya misitu na tumeshuhudia kuimarika kwa huduma za kitalii katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**,

Hayo yote yameweza kufanyika kutokana na kazi mbali mbali kama vile Doria 390 za kutafuta wahalifu (247 Unguja na 143 Pemba) zimefanyika katika maeneo ya rasimali za Misitu ambapo matukio 134 (64 Unguja na 70 Pemba) yaliripotiwa yanayohusu Uharibifu na ukataji wa Misitu pamoja na Usafirishaji wa mazao ya Misitu bila ruhusa.

**Mheshimiwa Spika**,

Fedha zilizoombwa na idara ya misitu ziingizwe kama walivyojipangia ili Idara iweze kuratibu shughuli walizojipangia ya kuimarisha upandaji wa miti kwa kuotesha miche 1,700,000 ya Misitu, Mikarafuu, Minazi, Matunda na Viungo ili kuzidisha thamani ya mazao haya pamoja na kuendeleza uwekezaji wa Miradi yenye tija katika hifadhi za misitu.

**Mheshimiwa Spika,**

Sote ni mashahidi, katika mwaka huu wa fedha tunaoumaliza tumeshuhudia idadi kubwa ya embe zimepatikana hususani katika kisiwa cha Pemba, hii imetokana na juhudi zilizofanywa za kampeni ya kudhibiti nzi waharibifu wa matunda ambapo jumla ya mitego 12408 ya dawa ya kunasia nzi wa matunda (ME) zimepelekwa kwa wakulima na lita 1,161 za dawa ya ‘Protein Bait GF 120 zimetolewa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati yetu katika ziara zake za kawaida imefuatilia na kuridhika na utaratibu unaotumika wa utowaji na upatikanaji wa huduma za mifugo ikiwemo dawa, chanjo na utoaji wa elimu juu ya ufugaji, uzalishaji na matumizi ya mbegu bora za mifugo jambo ambalo limesaidia wakulima wetu kuweza kufaidika na kazi wanazozifanya.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imekadiriwa kukusanya jumla ya TZS bilioni 8.241 kupitia vyanzo vyake 11 viliopo Unguja na Pemba. Kamati yetu hatuna pingamizi juu ya upatikanaji wa fedha hizo hivyo, tunaiomba Wizara kuzidisha umakini ili waweze kuzipata fedha hizo kwa asilimia moja.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunaipongeza idara ya umwagiliaji kwa miradi mizuri wanayoiratibu katika mabonde yetu ya mpunga. Tunawaomba wakulima wetu waisimamie miradi wanayopatiwa kwani fedha nyingi zimetumika wakati wa kuimarisha miradi hiyo. Tunatarajia kiwango cha fedha kilichoekwa kitaakisi kazi zilizopangwa za uendelezaji na uimarishaji wa miundombinu katika mabonde yetu kwa upande wa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Hatahivyo bado tunaendelea kupata malalamiko kutoka kwa wakulima wetu kuhusiana na vitendo vya baadhi ya wafugaji kuingiza wanyama katika mabonde hivyo, tunashauri Wizara itenge fungu kwa ajili ya kuimarisha ulinzi pamoja na kukaa na jumuiya za wafugaji na kuwapatia Elimu juu ya madhara ambayo yanaweza kujitokeza pindi mifugo hiyo ikiendelea kuzagaa ndani ya maeneo ya miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta iliomba kuidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 2.161 na mwaka huu wa fedha 2025/2026 wameomba **TZS bilioni 2.922** . Kuna ongezeko limejitokeza, Hivyo tunatarajia kuona utendaji kazi unazidi kuimarika kwavile ongezeko hilo litaenda kuimarisha mipango na mikakati bora kwavile wakulima wetu wanategemea sana huduma hizi za matrekta. Tuna imani kubwa mwaka huu mpya wa fedha2025/2026 mambo yatakua mazuri zaidi ili wakulima wetu wapate kunufaika kupitia Serikali yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi, Kamati yetu inaishauri Wizara kuweka utaratibu mzuri ili kuweza kuwafikia wakulima wote katika maeneo yao wanayofanya shughuli za kilimo ili kuepusha huduma hizi kukosekana kwa baadhi ya wakulima.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunazipongeza taasisi hizi na tunaziomba ziendeleze juhudi za kukusanya kwa lengo la kunyanyua uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha malengo ya Serikali katika utekelezaji wa programu zilizopangwa ndani ya bajeti hii yanafikiwa, Kamati inaamini kuwa malengo hayo yatafanikiwa endapo tu fedha zilizotengwa ndani ya bajeti tunayotegemea kuipitisha hapa zinapatikana kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inayasema hayo kutokana na uzowefu wa bajeti iliyopita ambapo baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo ilipangwa kutekelezwa katika mwaka huo wa fedha haijakamilika mpaka sasa kutokana na ukosefu wa fedha. Kamati inashangazwa na hali hiyo ambapo tunaamini kuwa wakati tunapitisha bajeti tulipanga kwa kujua fedha zipo na zitapatikana kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Biashara, Utalii na Kilimo ilipitisha bajeti ya Wizara hii kwa kutoa maelekezo na ushauri ambao Wizara iliahidi kuufanyia kazi ili malengo ya mwaka huu wa kibajeti yaweze kukamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo ,Umwagiliaji ,Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watumie fursa hii kuuliza, kujadili, kutoa mapendekezo yao na hatimaye kuipitisha Bajeti hii ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

……………………

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu,

M/Mwenyekiti,

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.